



NISHATI

HABARI ZA
NISHATI

News *Bulletin*

www.nishati.go.tz [Wizara ya Nishati](#) [wizara_ya_nishati_tanzania](#) [@Nishati2017](#) [Wizara ya Nishati](#)

Toleo Namba 27

Juni 1 - 30, 2021

RAIS SAMIA SULUHU HASSAN NA YOWERI KAGUTA MUSEVENI WASHUHUDIA UTIAJI SAINI MKATABA WA NCHI HODHI WA UJENZI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Uganda Yoweri Kaguta Museveni wakiwa wameshika nyaraka za Tamko la pamoja kuhusu utekelezaji wa pamoja wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima (Uganda) hadi Chongoleani Tanga (Tanzania) katika hafla iliyofanyika Ikulu Jijini Dar es Salaam



LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA
MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au
Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma

RAIS SAMIA SULUHU HASSAN NA YOWERI KAGUTA MUSEVENI WASHUHUDIA UTIAJI SAINI MKATABA WA NCHI HODHI WA UJENZI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiwa amesimama pamoja na Rais wa Uganda Yoweri Kaguta Museveni wakati wa nyimbo za Mataifa mawili ya Tanzania na Uganda zikipigwa katika viwanja vya Ikulu Jijini Dar es Salaam.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Jamhuri ya Uganda, Mhe. Yoweri Kaguta Museveni tarehe 20 Mei, 2021 walishuhudia utiaji saini wa mkataba hodhi wa ujenzi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki litakalojengwa kuanzia Hoima nchini Uganda hadi Bandari ya Tanga nchini Tanzania kati ya Serikali ya

Tanzania na Kampuni ya Mafuta Ghafi ya Afrika Mashariki (EACOP).

Hafu ya utiaji saini mkataba huo ilifanyika katika viwanja vya Ikulu Jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isidor Mpango, Mawaziri, viongozi wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama Wabunge, Makatibu Wakuu, wawakilishi kutoka kampuni za

uwekezaji wa CNOCC ya China na Total ya Ufaransa na wawakilishi kutoka Sekta binafsi.

Kwa upande wa Tanzania mkataba huo ulitiwa saini na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemmani na kushuhudiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali Prof. Adelardus Kilangi wakati upande wa kampuni ya EACOP umetiwa saini na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo Bw. Martin John Tiffen na

kushuhudiwa na Rais wa Utafti na Uzalishaji wa Total Afrika Bw. Nicolas Terraz.

Mhe. Waziri Kalemmani alisema utiaji saini wa mkataba huo umekamilisha hatua zote za majadiliano na sasa kinachoendelea ni kuanza kwa kazi za ujenzi wa bomba litakalokuwa na urefu wa kilometa 1,443 ambapo kati yake kilometa 1,147 zitajengwa katika ardhi ya Tanzania.

Ujenzi wa mradi huu



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Mhandisi Leonard Masanja
Katibu Mkuu

Makamu Mwenyekiti
Kheri Mahimbali

Mhariri
Dorina G. Makaya

Waandishi
Teresia Mhagama
Zuena Msuya
Hafsa Omar

Msanifu Kurasa
Lucas Gordon

Wasiliana nasi kwa simu
namba +255-26-2322018
Nukushi: +255-26-2320148
au

Fika Ofisi ya Mawasiliano
Mitumba Dodoma,
S.L.P 2494, Dodoma

 www.nishati.go.tz

 [Wizara ya Nishati](#)

 [@Nishati2017](#)

 [wizara_ya_nishati_tanzania](#)

 [Wizara ya Nishati](#)

Mradi wa Bomba la Mafuta kuleta neema kwa Watanzania

Hivi karibuni, Rais wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Uganda, Yoweri Kaguta Museveni walishuhudia utiaji saine wa mkataba hodhi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki, kati ya Serikali ya Tanzania na Kampuni ya Mafuta Ghafi ya Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi huo unahusisha ujenzi wa bomba hilo, litakalojengwa kuanzia Hoima nchini Uganda hadi bandari ya Tanga nchini Tanzania.

Hii ni hatua kubwa na ya kihistoria inayoimarisha pia uhusiano na ushirikiano wa kidugu uliopo, baina ya mataifa haya mawili jirani ambayo pia ni wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), lakini na historia ya kupambana na udhalimu.

Mradi huu si tu unaimarisha uhusiano wa kiuchumi na kijamii kati ya wananchi wa mataifa haya, lakini unaweka alama katika umoja, mshikamano na uimara wa Tanzania na Uganda, lakini pia na Afrika Mashariki yote.

Bomba hilo lenye urefu wa kilometa 1,443 huku kilometa 1,147 zikijengwa katika ardhi ya Tanzania, litagharimu dola bilioni 4.16 za Marekani na kusafirisha mapipa 216,000 ya mafuta ghafi kwa siku,

likihitaji vituo vinane.

Pia vitajengwa vituo 29 kwa ajili ya kulainisha mabomba ya chuma, valvu 76 na matanki matano yenye uwezo wa kuhifadhi mapipa 500,000 ya mafuta kila moja katika bandari ya Tanga.

Tanzania na Uganda kila moja inamiliki asilimia 15 ya hisa zote za kampuni hiyo, na kutokana na umiliki huo Tanzania itapata asilimia 60 ya mapato na Uganda itapata asilimia 40 na kutokana na mapato ya Dola za Marekani Milioni 290 zinazotarajiwa katika kipindi cha miaka 25 ya uhai wa mradi, Tanzania itapata mapato ya Dola za Marekani Milioni 59, itapata kodi ya kiasi cha Dola za Marekani Milioni 73, fedha za kigeni zitaongezeka kwa asilimia 53 na ajira zaidi ya 10,000 katika Mikoa 8, Wilaya 24, Kata 134, Vijiji 257 na Vitongoji 527 ambako bomba litapita.

Watanzania hatuna budi kushirikiana na Rais Samia Suluhu Hassan kuendeleza, kuenzi, kukuza na kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa kirafiki, kidugu na kihistoria, kati ya Tanzania na Uganda, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha mradi unafanikiwa kwa manufaa ya wananchi wa nchi hizi mbili.

RAIS SAMIA SULUHU HASSAN NA YOWERI KAGUTA MUSEVENI WASHUHUDIA UTIAJI SAINI MKATABA WA NCHI HODHI WA UJENZI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI

INATOKA UK.2

unaotarajiwa kugharimu Dola za Marekani Bilioni 4.16 utakamilika katika kipindi cha miaka 3 ambapo utakuwa na uwezo wa kusafirisha mapipa 216,000 ya mafuta ghafi kwa siku, utahusisha ujenzi wa vituo 8, ujenzi wa vituo vya kulainisha mabomba

ya chuma 29, ujenzi wa valvu 76 na ujenzi wa matanki 5 yenye uwezo wa kuhifadhi mapipa laki 5 ya mafuta kila moja katika Bandari ya Tanga.

Tanzania na Uganda kila moja inamiliki asilimia 15 ya hisa zote za kampuni hiyo, na kutokana na umiliki huo Tanzania itapata asilimia

60 ya mapato na Uganda itapata asilimia 40 na kutokana na mapato ya Dola za Marekani Milioni 290 zinazotarajiwa katika kipindi cha miaka 25 ya uhai wa mradi, Tanzania itapata mapato ya Dola za Marekani Milioni 59, itapata kodi ya kiasi cha Dola za Marekani Milioni 73, fedha za

kigeni zitaongezeka kwa asilimia 53 na ajira zaidi ya 10,000 katika Mikoa 8, Wilaya 24, Kata 134, Vijiji 257 na Vitongoji 527 ambako bomba litapita.

Katika hotuba yake, Mhe. Rais Samia alimshukuru aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Magufuli aliyeanza mchakato wa mradi huo pamoja na Mhe. Rais Museveni, aliwapongeza Mawaziri, Makatibu Wakuu na kamati za majadiliano za Tanzania na Uganda kwa kufanikisha kuanza kwa mradi huo.

Aliahidi kuwa Tanzania itaendeleza, kuenzi, kuukuza na kuuimarisha uhusiano na ushirikiano wa kirafiki, kidugu na kihistoria kati yake na Uganda ikiwa ni pamoja na kuhakikisha mradi huo unafanikiwa kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania na Uganda.

Mhe. Rais Samia alisema anaamini kuwa, mradi huo utachochea



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akishuhudia utiaji saini wa Mkataba wa Nchi hodhi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima (Uganda) hadi Chongoleani Tanga (Tanzania) katika hafla iliyofanyika Ikulu Jijini Dar es Salaam. Wanaosaini ni Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani na kushuhudiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali Prof. Adelarudus Kilangi wakati upande wa kampuni ya EACOP anayetia saini ni Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo Bw. Martin John Tiffen na kushuhudiwa na Rais wa Utafiti na Uzalishaji wa Total Afrika Bw. Nicolas Terraz.

RAIS SAMIA SULUHU HASSAN NA YOWERI KAGUTA MUSEVENI WASHUHUDIA UTIAJI SAINI MKATABA WA NCHI HODHI WA UJENZI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiwa katika mazungumzo na mgeni wake Rais wa Uganda Yoweri Kaguta Museveni mara baada ya kuwasili katika Viwanja vya Ikulu Jijini Dar es Salaam tarehe 20 Mei, 2021.

juhuri za pamoja za utafutaji mafuta na gesi katika nchi za ukanda huu zikiwemo Tanzania, DRC, Burundi na Sudan Kusini na pia utawavutia wawekezaji wengi zaidi kuja kuwekeza Tanzania na nchi nyingine za ukanda huu.

Kwa upande wake, Mhe. Rais Museveni alisema moja ya changamoto kubwa alizoziona katika safari yake ya kupigania ukombozi na maendeleo ya Afrika ni kukosekana kwa mwelekeo lakini kuanza kwa mradi huo ni uthibitisho kuwa sasa mwelekeo unaonekana.

Alifanua kuwa, katika kutafuta ustawi

wa jamii, pamoja na kusimamia sekta za huduma za jamii zinazojumuisha elimu, afya, maji na usalama ni lazima kusimamia uzalishaji mali

utakaosaidia kupata utajiri na fedha kama vile kilimo, viwanda, huduma na tehama ambazo kwa pamoja zinahitaji uwepo wa miundombinu bora na nishati.

Hata hivyo, Mhe. Rais Museveni alionya kuwa, mradi wa bomba la mafuta usisababisha Tanzania na Uganda kubweteka na kuacha kusimamia ipasavyo sekta za kudumu za uzalishaji mali kwa kuwa mafuta yana mwisho.

Mhe. Rais Samia na Mhe. Rais Museveni walitia saini tamko la pamoja la utekelezaji wa mradi huo (Communiqué) na kisha Mhe. Rais Museveni alirejea nchini Uganda.

CHANZO;
www.ikulu.go.tz



Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Philip Isidor Mpango akipiga makofi pamoja na viongozi wengine wa ndani na nje ya Nchi mara baada ya hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan Ikulu Jijini Dar es Salaam.

Umeme wa JNHPP kuanza kutumika Juni 2022



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) na Waziri wa Nyumba na Maendeleo ya Makazi wa Misri, Dkt. Assem El- Gazzar wakikagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere wakati wa ziara yao iliyofayika Mei 22, 2021, mkoani Pwani.

Zuena Msuya, Pwani

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard

Kalemani amewaeleza wataanzania kuwa, mradi wa kufua Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) utaanza kuzalisha Umeme utakaotumika katika gridi ya taifa kuanzia mwezi Juni 2022 kwa kuwa hatua ya ujenzi ya maeneo muhimu ya kuzalisha umeme yamefikia 52.8% mpaka sasa.

Dkt. Kalemani alisema hayo wakati wa ziara yake na Waziri wa Nyumba na Maendeleo ya Makazi wa Misri, Dkt. Assem El- Gazzar ya kukagua maendeleo na

ya ujenzi wa mradi huo, iliyofayika Mei 22, 2021, mkoani Pwani.

Dkt. Kalemani alisema kuwa kazi ya ujenzi wa mradi huo inaendelea vizuri na kwamba wataanzania wataanza kunufaika kwa kutumia Umeme unaozalishwa katika bwawa hilo mwezi Juni mwakani.

Alisema kuwa, katika kuhakikisha mradi huo unakamilika ndani ama kabla ya muda uliopangwa, amewataka wahandisi wote wa kampuni inayotekeleza mradi huo kuishi ndani ya eneo la mradi ili kufanya kazi hiyo usiku na mchana.

“Ujenzi wa ukuta wa kingo ya kuzuia maji kwenye bwawa unaendelea vizuri,

kuanzia Novemba Mwaka huu tutaanza kujaza Maji katika bwawa letu na hadi kufika Aprili mwakani tayari maji yatakuwa yamejaa kufikia kiwango cha kutosha kuzalisha umeme, mwezi Mei 2022 tutafanya majaribio ya mitambo ya kuzalisha umeme na mwezi Juni tutaanza kuzalisha umeme utakaoingizwa katika Gridi ya taifa kwa matumizi.” Alisema Dkt. Kalemani

Hata hivyo Dkt. Kalemani alieleza kuwa, tayari mashineumba (Transfoma) 6 kati ya 27 zitakazotumika kuongezea nguvu ya umeme pindi utakapoanza kuzalishwa zimeshawasili nchini huku nyingine zikiwa

mbioni kufika.

Aliagiza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuwa, ndani ya siku 7 kuanzia sasa ihakikishe inakamilisha taratibu zote za kuwezesha mitambo hiyo kutoka bandarini na kufikishwa katika eneo la mradi ili kuanza kufungwa katika maeneo husika.

Sambamba na hilo, alieleza kuwa, baadhi ya wataalam wako nchini China kukagua baadhi ya mitambo mingine inayotengenezwa huko kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo mkubwa wa kuzalisha umeme.

Alisema kuwa, mpaka sasa tayari mkandarasi anayetekeleza mradi huo ameshalipwa kiasi cha shilingi Trilioni 2.43 na fedha hizo zimekuwa



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kushoto) na Waziri wa Nyumba na Maendeleo ya Makazi wa Misri, Dkt. Assem El- Gazzar (kulia) wakiteta jambo wakati wa kikao kabla ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere wakati wa ziara yao iliyofanyika Mei 22, 2021, mkoani Pwani.

Umeme wa JNHPP kuanza kutumika Juni 2022



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akimuonyesha sehemu ya mradi Waziri wa Nyumba na Maendeleo ya Makazi wa Misri, Dkt. Assem El- Gazzar (kulia) wakati wa kukagua maendeleo na hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa JNHPP.

zikilipwa kwa wakati.

Aliweka wazi kuwa, Serikali haitamvumilia yeyote atakayejaribu ama kusababisha mradi huo kutokamilika kwa wakati kwa kuwa kila kitu kimekuwa kikitekelezwa kwa kuzingatia misingi ya mkataba, na atakayebainika kufanya hivyo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Kwa upande wake Waziri wa Nyumba na Maendeleo ya Makazi wa Misri, Dkt. Assem El-Gazzar alimhakikishia Dkt. Kalemani kuwa mradi huo utakamilika ndani ya muda uliopangwa, na kwamba kwa kufanya hivyo kutazidi kuimarisha mahusiano mazuri kati ya nchi hizo mbili.



Kazi ya ujenzi ikiendelea katika mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere uliopo mkoani Pwani.

Dkt. El – Gazzar alisema kuwa watakapokamilisha mradi huo kama ilivyopangwa, nchi yake itakuwa katika nafasi nzuri ya kuendelea kuwekeza Tanzania kwa kupata kazi ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Aidha alisema Serikali yake itaendelea kuimarisha usimamizi wa mradi huo na kwamba watahakikisha watalaam

wote wanaotakiwa katika kila hatua ya kutekeleza mradi huo wanafika kwa wakati nchini na kutimiza majukumu yako kama inavyotakiwa.

Dkt. El-Gazzar aliambatana na ujumbe wa watu zaidi ya 50, na hii ikiwa ni mara yake ya nne kutembelea mradi huo tangu ulipoanza kutekelezwa mwaka 2019, huku Dkt.Kalemani ikiwa ni mara yake ya 16 kutembelea mradi huo.



Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga (kulia) na Mwakilishi wa Mhandisi Mkazi wa Mradi wa JNHPP, Mhandisi Lutengano Mwandambo (kushoto), wakizungumza wakati ziara ya kukagua maendeleo ya Ujenzi wa mradi wa Julius Nyerere iliyofayika Mei 22, 2021, mkoani Pwani.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) na Waziri wa Nyumba na maendeleo ya Makazi wa Misri, Dkt. Assem El- Gazzar (kushoto kwa Waziri Dkt. Kalemani) wakiwa katika picha ya pamoja na ujumbe ulioambatana na Waziri wa Misri wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere.

Kituo kipya cha umeme Mtera kikamilike kabla ya Oktoba – Naibu Waziri Byabato



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (wa kwanza kutoka kulia) akikagua moja ya transformita itakayofungwa katika kituo kipya cha kupoza umeme cha Mtera.

Na Teresia Mhagama

Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato ameagiza kuwa, ujenzi wa kituo kipya cha kupoza umeme cha kV 220/33 katika Kituo cha umeme cha Mtera ukamilike kabla ya mwezi Oktoba mwaka huu.

Alitoa agizo hilo tarehe 9 Mei, 2021 wakati alipofanya ziara katika kituo cha kufua cha umeme cha Mtera na kukagua sehemu ya Bwala la Maji la Mtera, kazi ya uzalishaji umeme na maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho kipya cha kupoza umeme ambapo aliambatana na

Watendaji kutoka Wizara ya Nishati, Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na TANESCO.

“Tunapanua kituo cha kupoza umeme kilichopo hapa ili kukiongezea nguvu na hivyo kuweza

kusambaza umeme katika Mkoa wa Iringa na Dodoma, kazi ilichelewa kidogo kutokana na masuala mbalimbali ikiwemo upatikanaji wa vifaa vya umeme kutoka nje ya nchi, hivyo nimetoa maelekezo kuwa Mkandarasi anatakiwa kufanya kazi usiku na mchana.” Alisema Wakili Byabato

Alieleza kuwa, tayari baadhi ya kazi zimeshafanyika katika kituo hicho kipya cha kupoza umeme ikiwemo ujenzi wa miundombinu na ufikishaji wa transformita na vifaa vingine vya umeme vinavyohitajika.

Kuhusu hali ya

uzalishaji umeme katika Kituo cha Mtera, alisema kuwa, kituo hicho kinazalisha megawati zote 80 kutoka katika mitambo miwili iliyopo kituoni hapo ambapo kila mtambo unazalisha megawati 40, hivyo aliwapongeza watalaam wa TANESCO kwenye kituo hicho kwa kufanya kazi kwa weledi, kujituma na ubunifu.

Aidha, alisema kuwa, kuna maji ya kutosha kuzalisha umeme katika Bwala la Mtera, yenye kina cha mita 698.50 na kwamba maji yaliyopo yana uwezo wa kuzalisha umeme katika kipindi cha mwaka mzima hata kama mvua



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (wa kwanza kutoka kulia) akiangalia kiwango cha maji katika Bwala la Mtera ambayo yanatumika kuzalisha umeme wa kiasi cha megawati 80 katika Kituo cha kufua umeme cha Mtera. Kushoto kwake ni Meneja wa Kituo cha kufua umeme cha Mtera, Elias Mwalukilo.

Kituo kipya cha umeme Mtera kikamilike kabla ya Oktoba – Naibu Waziri Byabato



Kaimu Mhandisi Mkuu katika Kituo cha kufua umeme cha Mtera, Phesto Chikongoye (kushoto) akitoa maelezo kwa Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato kuhusu uendeshaji wa mitambo mbalimbali ya umeme katika kituo hicho.



Baadhi ya mitambo ya kuzalisha umeme iliyopo katika kituo cha kufua umeme cha Mtera.

hazitanyesha.

Vilevile alisema kuwa, Serikali inatilia mkazo suala la ujenzi wa miundombinu ya umeme ili kuweza kuwafikishia umeme wananchi wengi zaidi na alitoa rai kwa wananchi kulinda miundombinu ya umeme na kuunganisha umeme mara unapofika kwenye maeneo yao.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mhandisi Jones Olotu, alisema kuwa, watamsimamia mkandarasi aliyepewa kazi ya ujenzi kituo kipya cha kupoza umeme cha Mtera ili kuhakikisha kuwa kazi husika inakamilika mwezi Septemba kama ambavyo imeagizwa na

Naibu Waziri.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri wa Nishati, alikagua kazi ya ujenzi wa miundombinu ya umeme katika kijiji cha

NhiNhi kilichopo wilayani Chamwino, Mkoa wa Dodoma na kumuagiza mkandarasi, kampuni ya A to Z, kupeleka umeme kwenye kijiji hicho kabla

ya tarehe 30 Juni mwaka huu, na umeme huo ufike kwenye Taasisi zote za umma ikiwemo Shule na Kituo cha Afya.



Baadhi ya mitambo ya umeme katika kituo cha kupoza umeme cha Mtera.

Miradi ya REA III mzunguko wa Pili na PERI URBAN kwa Kanda ya Kaskazini, yazinduliwa

**Na Zuena Msuya,
Arusha**

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard

Kalemani amezindua rasmi Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini Awamu ya Tatu (REA III) mzunguko wa Pili na ule wa Usambazaji wa Umeme kwa Vijiji vilivyoko Pembezoni mwa Miji (PERI URBAN) kwa mikoa ya Kanda ya



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akikabidhi kifa cha Umeme Tayari (UMETA) kwa Wakazi wa Kijiji cha Kiseriani katika Kata ya Engikageti wilayani Longido mkoani Arusha, wakati wa uzinduzi wa Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu (REA III) mzunguko wa pili kwa Kanda ya Kaskazini uliofanyika mkoani humo, Mei 23, 2021.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza na Wakazi wa Kijiji cha Terati katika Wilaya ya Arusha Jiji wakati wa uzinduzi Mradi wa Kusambaza umeme katika Vijiji vilivyo pembezoni mwa Miji (PERI URBAN) kwa Kanda ya Kaskazini uliofanyika mkoani Arusha, Mei 23, 2021.

Kaskazini.

Uzinduzi huo ulifanyika mkoani Arusha katika wilaya mbili tofauti, ambapo mradi wa REA III mzunguko wa pili ulizinduliwa katika Kijiji cha Kiseriani Kata ya Engikageti wilayani Longido na PERI URBAN ilizinduliwa katika Kijiji cha Terati Wilaya ya Arusha, Mei 23, 2021. Kanda ya Kaskazini inahusisha Mikoa minne ambayo ni Kilimanjaro,

Arusha, Tanga na Manyara.

Akizungumza kwa nyakati tofauti wakati akizindua mradi huo, Dkt. Kalemani aliwataka wakazi wa maeneo husika kuanza kutandaza nyaya katika nyumba zao ili kujiandaa kuunganishiwa umeme katika nyumba zao wakati wakandarasi wakifanya kazi ya kuusambaza katika maeneo yao.

Miradi ya REA III mzunguko wa Pili na PERI URBAN kwa Kanda ya Kaskazini, yazinduliwa



Wakazi wa Kijiji cha Kiseriani katika Kata ya Engikageti wilayani Longido mkoani Arusha wakimsikiliza Waziri wa Nishati (hayupo pichani), wakati wa uzinduzi rasmi wa Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu (REA III) mzunguko wa pili kwa Kanda ya Kaskazini uliofanyika mkoani humo, Mei 23, 2021.

Aidha aliwaeleza wananchi hao kuwa gharama za

kuunganishiwa umeme huo ni shilingi 27,000 na kwamba wasikubali

kutozwa gharama zaidi na watu wasio waaminifu.

“Watanzania kwa sasa suala la kuweka umeme ni lazima ndugu zangu, Serikali imeamua kubeba gharama zote na kuwataka kuchangia shilingi 27,000 tu, hii ni kuhamasisha kila mwananchi aunganishiwe umeme, utakuwa mtu wa ajabu serikali imeleta umeme katika eneo lako na kwa bei nafuu halafu wewe usiweke umeme tutakushanga kwakweli, hii fursa itumieni vizuri.” Alisisitiza Dkt. Kalemani.

Dkt. Kalemani aliweka wazi kuwa, mradi wa REA III mzunguko wa pili mkoani humo utatekelezwa ndani ya kipindi cha miezi 18 na utatekelezwa na kampuni ya SAGEMCOM kutoka nchini Ufaransa na mradi wa Peri Urban utatekelezwa ndani ya kipindi cha miezi 12 na Kampuni ya DERM ambayo ni ya Kitanzania.

Hata hivyo aliwaeleza wakandarasi

Miradi ya REA III mzunguko wa Pili na PERI URBAN kwa Kanda ya Kaskazini, yazinduliwa

wanaotekeleza miradi hiyo, kufanya kazi usiku na mchana ili kumaliza kazi hiyo hata kabla ya muda uliopangwa, na kwamba wachukue vijana kutoka kila eneo husika ili kutekeleza kazi za uchimbaji wa mashimo, kusimika nguzo na kufunga nyaya ili na wao wanufaike na uwepo wa mradi huo.

Aliwaeleza wakandarasi hao kuwa, Serikali haitaongeza muda wa ziada kwa mkandarasi yeyote atakayechelewa kukamilisha mradi huo kwa wakati uliopangwa, na kwamba ikitokea mkandarasi akafanya hivyo atakatwa asilimia 10 ya fedha zake ikiwa ni adhabu kama makubaliano ya mkataba yanavyoelekeza.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijiji (REA), Mhandisi Amos Maganga aliwaeleza wakandarasi hao

kuwa wanatakiwa kujitambulisha kwa uongozi wa ngazi za Wilaya, Kijiji na Kata kabla ya kuanza kazi zao ili wafahamike na kupewa ushirikiano.

Vilevile aliwataka wananchi kushirikiana vyema na wakandarasi

hao ili waweze kufanya kazi zao kwa urahisi, na kwamba wanakijiji wawe walinzi wa miundombinu ya umeme pamoja na vifaa vitakavyokuwa vikitumika.

Aidha aliwasisitiza wananchi kuwa gharama za kutandaza nyaya

katika nyumba zao ni makubaliano kati yao na fundi atakayetekeleza kazi hiyo, pia aliwataka kuwatumia mafundi walioidhinishwa na Shirika la umeme Tanzania (TANESCO) kufanya kazi hiyo.



Wazee wa Kimila (kushoto) wa Kijiji cha Terati katika Wilaya ya Arusha Mji wakimkabidhi zawadi Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (kulia) baada ya kumsimika na kumpa jina la Ole Kalemani wakati wa uzinduzi rasmi Mradi wa Kusambaza umeme katika vijiji vilivyo pembezoni mwa miji (PERI URBAN) kwa Kanda ya Kaskazini uliofnyika mkoani Arusha, Mei 23, 2021.

WATUMISHI WA WIZARA YA NISHATI IDARA YA PETROLI NA GESI WATEMBELEA MRADI WA GESI SONGOSONGO

**Hafsa Omar -
Songo Songo**

Watumishi wa Wizara ya Nishati, wa Idara ya Petroli na Gesi, wametembelea Kiwanda cha kuchakata gesi kilichopo katika kisiwa cha Songo Songo, kata ya Songo Songo wilayani Kilwa, Mkoa wa Lindi.

Ziara hiyo iliyokuwa na lengo la kukagua maendeleo ya kazi katika kiwanda hicho, iliongozwa na Kamishna Msaidizi wa Gesi, Mhandisi Mohamed Fakihi aliyeambatana na Mhandisi Rabia Issa na Mhandisi Anita Ringia.

Wakiwa katika ziara hiyo watumishi hao walitembelea sehemu mbalimbali katika kiwanda hicho ambapo walijionea kazi mbalimbali zinazofanywa

kiwandani hapo.

Akizungumza na Watumishi wa kiwanda hicho, Mhandisi Fakihi, aliwaeleza kuwa lengo la ziara hiyo ni kujionea maendeleo ya uendeshwaji wa kiwanda hicho na kusema kuwa ameridhishwa na utendaji kazi wa watumishi hao na kuwataka kuendelea kufanya kazi kwa juhudi ili Watanzania waendeleo kunufaika na mradi huo.

Naye, Mhandisi

Cosmas Kachacha ambaye ni Kaimu Meneja wa Kiwanda hicho, alisema amefurahishwa na ujio watumishi hao kutoka wizarani ambapo alieleza kuwa ujio huo una manufaa makubwa kwa kiwanda hicho.

Alisema kuwa, ziara za Watumishi hao zinaimarisha uhusiano Kati ya Wizara na Taasisi zake na hivyo kuboresha utendaji wa kazi.



Picha mbalimbali za ziara ya watumishi wa Wizara ya Nishati katika kiwanda cha kuchakata Gesi Asilia Songosongo

Wakandarasi wa mradi wa REA III mzunguko wa Pili watakiwa kwenda maeneo ya kazi



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza na wakandarasi wa mradi wa usambazaji umeme Vijijini wa Awamu ya Tatu, mzunguko wa Pili (hawapo pichani). Kushoto kwake ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato.

Styden Rwebangila, Watendaji Wakuu wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) pamoja na wasimamizi wa miradi ya REA kutoka Wizara ya Nishati, TANESCO na REA.

“Tunataka wakandarasi muwe kwenye maeneo yenu ya kazi, na wale wakandarasi kutoka nje ya nchi muwe na ofisi zenu hapa nchini, hatuwezi tukawapa ninyi kazi na mnaachia vibarua

Na Teresia Mhagama, Dodoma

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani amefanya kikao kazi na wakandarasi kutoka kampuni 34 waliopewa kazi na Serikali ya kusambaza umeme katika vijiji vyote ambavyo bado havina umeme kupitia mradi wa usambazaji umeme

vijijini wa Awamu ya Tatu mzunguko wa Pili na kuwaagiza kwenda kwenye maeneo yao ya kazi.

Kikao kazi hicho kilifanyika tarehe 25 Mei, 2021 na kuhudhuriwa na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Naibu Katibu Mkuu, Kheri Mahimbali, Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Edward Ishengoma, Kamishna Msaidizi wa Maendeleo ya Nishati, Mhandisi



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akizungumza wakati wa kikao na wakandarasi wa mradi wa usambazaji umeme Vijijini wa Awamu ya Tatu, mzunguko wa Pili (hawapo pichani). Kulia kwake ni Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani na kushoto kwake ni Kamishna Msaidizi wa Maendeleo ya Nishati, Mhandisi Styden Rwebangila.

Wakandarasi wa mradi wa REA III mzunguko wa Pili watakiwa kwenda maeneo ya kazi

tu kuwa kwenye maeneo ya kazi huku wakiwa hawana mamlaka, na nyie wakurugenzi ambao kampuni zenu ni za hapa nchini pia mhakikishe mnakuwepo kwenye maeneo ya kazi." Alisema Dkt.Kalemani.

Waziri wa Nishati alitumia kikao kazi hicho kuwapa maelekezo mahususi wakandarasi hao ili mradi huo uweze kufanyika kwa ufanisi

ikiwemo kuwataka kufanya kazi kwa kasi, ubunifu na usahihi wenye weledi pamoja na masharti mengine yaliyo kwenye mikataba yao.

Kuhusu kufanya kazi kwa kasi, alisema kuwa wakandarasi hao wanapaswa kufanya kazi na kumaliza ndani ya muda, ambao ni miezi 18 au kabla ya hapo.

Katika suala la ubunifu, aliwataka



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza na wakandarasi wa mradi wa usambazaji umeme Vijijini wa Awamu ya Tatu, mzunguko wa Pili (hawapo pichani). Kulia kwake ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali.

wakandarasi hao kukidhi

mahitaji ya wananchi kwani wanachohitaji wananchi hao ni umeme na sio kuona tu miundombinu ya umeme inapita.

Vilevile kuhusu usahihi, alisema kuwa Serikali inategemea kuona thamani ya pesa inayotumika kwenye mradi huo na ishara mojawapo ni umeme kuunganishwa kwa wananchi wengi na Taasisi za umma.

Aidha, Dkt.Kalemani aliagiza kila mkandarasi anapofika kwenye eneo lake la kazi atoe taarifa kwa uongozi wa eneo husika ikiwemo Wakuu



Baadhi ya Mameneja wa TANESCO kutoka sehemu mbalimbali nchini pamoja na Wakandarasi wa mradi wa usambazaji umeme vijijini wa Awamu ya Tatu, mzunguko wa Pili wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani (hayupo pichani) wakati alipofanya kikao na wakandarasi hao jijini Dodoma.

Wakandarasi wa mradi wa REA III mzunguko wa Pili watakiwa kwenda maeneo ya kazi



Baadhi ya Wasimamizi wa Miradi ya usambazaji umeme vijijini kutoka Wizara ya Nishati, watendaji wa REA, TANESCO na wakandarasi wa mradi wa usambazaji umeme vijijini wa Awamu ya Tatu mzunguko wa Pili wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) jijini Dodoma.

wa Wilaya na Wawakilishi wa wananchi jambo litakalopelekea kazi zao kufanyika kwa ufanisi.

Pia, ameagiza vifaa vya kazi vitakavyotumika kwenye mradi huo viwe bora na isije kutokea wananchi wanawashiwa umeme leo halafu kesho vifaa kama vile transfoma vinaharibika.

Sanjari na hilo, alitoa agizo, vifaa vinavyopatikana ndani ya nchi ndivyo vitumike kwenye mradi huo wa REA III mzunguko wa Pili ikiwemo nyaya, transfoma na nguzo ili

kuwahisha kazi na kutoa ajira kwa wananchi.

Vilevile, alielekeza wakandarasi kuweka magenge mengi ya kazi na yasipungue matano kwenye kila eneo wanalofanyia kazi na pia watumie vijana wanaotoka katika maeneo wanayofanyia kazi.

Suala la kuwacheleweshea umeme wananchi waliolipia huduma ya umeme, aliagiza kuwa, lisiendelee na wananchi waunganishiwe umeme ndani ya siku 14 baada

ya kufanya malipo.

Dkt.Kalemani pia aliziagiza TANESCO na REA kuwasimamia wakandarasi na kuwakagua muda wote, kuwawekea mazingira wezeshi ya kufanya kazi zao na kuchukua hatua kwa mujibu wa mikataba.

Waziri wa Nishati pia alielekeza kuwa, wakandarasi lazima wawe na maeneo ya kuweka vifaa vya kazi, wasiuzie nguzo wananchi na wakandarasi wanaotandaza nyaya za umeme kwenye nyumba za wananchi, lazima wajulikane na REA, TANESCO ili kuepusha wananchi kutapeliwa, kufanyiwa kazi chini ya viwango na kupewa gharama zisizo stahiki.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato alisema kuwa, atahakikisha lengo na adhama ya Serikali ya kuwa, ifikapo mwaka 2022 kila kijiji nchini kinapata umeme

linafikiwa na kwamba maelekezo aliyoyatoa Waziri wa Nishati ni mahsusi na yanapaswa kufanyiwa kazi ili kufikia lengo tajwa.

Alisisitiza pia kuhusu wakandarasi kutoa taarifa kwa wawakilishi wa wananchi na viongozi mbalimbali mara wanapokuwa katika maeneo ya kazi.

Aidha, aliagiza kuwa, Wakandarasi waweke utaratibu wa wananchi kulipia kidogo kidogo gharama za kuunganisha umeme vijijini ili waweze kupata huduma hiyo kwani wengine hawana uwezo wa kulipa shilingi 27,000 kwa mkupuo, akitoa mfano kuwa, fedha hizo zinaweza kulipwa ndani ya mwezi.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali alisema kuwa, Wizara imepokea maelekezo yote yaliyotolewa kwenye kikao hicho na itasimamia utekelezaji wake.

Dkt. Kalemani na Wadau wajadili biashara ya mafuta



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati), akizungumza na wadau wa mafuta nchini, wakati wa mkutano wa kujadili mambo mbalimbali yanayohusu biashara ya mafuta nchini, kulia ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, na Mwenyekiti chama cha Wafanyabiashara ya Mafuta nchini (TAOMAC), Orando Da' Costa (kushoto), mkutano huo ulifanyika jijini Dar es Salaam, Mei 21, 2021.

Na Zueni Msuya, DSM

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard

Kalemani amekutana

na Wadau wa Mafuta nchini na kujadiliana mambo kadhaa yanayohusu biashara hiyo na kuunda timu ya watu kumi itakayofikisha mapendekezo ya wadau hao serikalini, ya namna

bora ya watanzania kushiriki katika biashara ya uagizaji wa mafuta kutoka nje ya nchi.

Aidha timu hiyo pia itapendekeza njia bora ya uwekaji wa vinasaba katika mafuta nchini

ili kudhibiti biashara hiyo ambapo Timu hiyo itafanya kazi kwa muda wa miezi mitatu.

Majadiliano hayo yalifanyika jijini Dar es Salaam ambapo Mkutano huo ulihudhuriwa na



Baadhi ya wadau wa mafuta nchini wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) wakati wa mkutano wa kujadili mambo mbalimbali yanayohusu biashara ya mafuta nchini, ulifanyika jijini Dar es Salaam, Mei 21, 2021.

Dkt. Kalemani na Wadau wajadili biashara ya mafuta

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, Kaimu Kamishna wa Mafuta na Gesi, Sebastian Shana na viongozi wengine kutoka wizara.

Wajumbe wa timu hiyo ni kutoka Wizara ya Nishati, Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa pamoja (PBPA), Chama Wafanyabiashara ya Mafuta nchini (TAOMAC) na Chama cha Wamiliki wa Vituo vya Mafuta Tanzania (TAPSOA).

Katika Mkutano huo, Dkt. Kalemani aliwaeleza wadau wa mafuta kuwa tokea mwezi Aprili mwaka huu, Serikali kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ndiyo mwenye dhamana ya kuweka vinasaba katika mafuta yote yanayoagizwa na kutumika hapa nchini tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo kazi hiyo ilikuwa ikifanywa na



Kaimu Mkurugenzi mtendaji wa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa pamoja (PBPA) Erasto Simon, (kushoto), Kaimu Kamishna wa Mafuta na Gesi, Sebastian Shana (pili kushoto) na wawakilishi kutoka Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), wakiwasikiliza wadau wa mafuta hawapo pichani wakati mkutano wa kujadili mambo mbalimbali yanayohusu biashara ya mafuta nchini, uliofanyika jijini Dar es Salaam, Mei 21, 2021.

kampuni ya nje.

Aliweka wazi kuwa kwa sasa Serikali inaangalia njia bora, rahisi ya haraka na gharama nafuu kwa kuweka vinasaba katika kila mafuta yanayoingia na kutumiwa hapa nchini ili kuendelea kuimarisha ubora wa mafuta.

Hata hivyo aliendelea kusema kuwa, lengo la Serikali ni kuimarisha mashirika yake ya ndani na kuwaongezea watanzania uwezo na ujuzi wa kufanya kazi mbalimbali kwa manufaa

ya taifa.

Kwa upande wao wadau wa mafuta, waliipongeza Serikali kwa hatua yake ya kuitumia TBS katika kuweka vinasaba katika mafuta yanayoingia na kutumika nchini jambo ambalo limepunguza ukiritimba katika kazi hiyo.

Pamoja na mambo mengine, wameomba Serikali kuliongezea uwezo shirika hilo, ili liweze kufanya kazi zake kwa ubora wa hali ya juu na ufanisi mkubwa katika

kudhibiti viwango na ubora wa mafuta nchini.

Aidha, Dkt. Kalemani aliendelea kuwasisitiza wafanyabiashara ya mafuta nchini kufungua vituo vidogo vya mafuta vijijini ili kusogeza karibu huduma ya nishati hiyo kwa wananchi na kwamba tayari EWURA wamepitia upya kanuni ya biashara ya mafuta na kuifanyia maboresho ili kuruhusu vituo hivyo kujengwa.

Mradi wa usambazaji umeme wa REA III mzunguko wa Pili mkoani Geita wazinduliwa

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard

Kalemani amezindua mradi wa usambazaji umeme vijijini wa Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili mkoani Geita unaotarajiwa kusambaza umeme katika vijiji 117 ambavyo bado havina umeme mkoani humo.

Uzinduzi huo uliofanyika katika Kijiji cha Mpakali wilayani Mbogwe, mkoani Geita tarehe 17 Mei, 2021 ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali

wakiwemo Mbunge wa Mbogwe, Nicodemus Maganga, Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe, Martha Mkupasi, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Julius Kalolo, Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mhandisi Amos Maganga na watendaji wengine kutoka Wizara ya Nishati na TANESCO.

“Katika Mkoa wa Geita, kuna vijiji 117 ambavyo bado havina umeme kati ya Vijiji takriban 474 na katika Wilaya ya Mbogwe, Vijiji 33 tu bado havina umeme kati ya Vijiji 87, hivyo leo tumeanza



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani pamoja na viongozi mbalimbali kutoka wilayani Mbogwe mkoani Geita, TANESCO na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), wakikata utepe kuashiria uzinduzi wa Mradi wa Usambazaji umeme vijijini wa Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili mkoani Geita.

kuleta wakandarasi watakaoanza kazi ya kupeleka umeme katika vijiji ambavyo bado havina umeme kwa

kuanzia hapa Mpakali.” Alisema Dkt.Kalemani Alieleza kuwa, mradi huo utatekelezwa katika kipindi cha miezi 18 na Serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni 75.6 kwa ajili ya shughuli hizo za usambazaji umeme vijijini mkoani Geita.

Aidha, ili miradi ya umeme vijijini iweze kuwa na tija, Dkt. Kalemani aliwahimiza wananchi kote nchini kuhakikisha kuwa wanaunganisha umeme mara unapofika kwenye maeneo yao kwani Serikali inatumia fedha nyingi kufikisha miundombinu ya umeme sehemu mbalimbali nchini.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (mbele, kulia) pamoja na viongozi mbalimbali kutoka wilayani Mbogwe mkoani Geita, TANESCO na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), wakifunua kitambaa kuashiria uzinduzi wa Mradi wa Usambazaji umeme vijijini wa Awamu ya Tatu, mzunguko wa Pili mkoani Geita.

Mradi wa usambazaji umeme wa REA III mzunguko wa Pili mkoani Geita wazinduliwa



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani pamoja na viongozi mbalimbali kutoka wilayani Mbogwe mkoani Geita, TANESCO na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), wakikata utepe kuashiria uzinduzi wa umeme katika Kijiji cha Nyakasaluma wilayani Mbogwe. Kijiji hicho kimesambaziwa umeme kupitia mradi wa usambazaji umeme vijijini wa Awamu ya Tatu, Mzunguko wa kwanza.

Miundombinu ya umeme katika Shule ya Msingi Nyakasaluma wilayani Mbogwe. Kijiji hicho kimesambaziwa nishati ya umeme kupitia mradi wa usambazaji umeme vijijini wa Awamu ya Tatu, Mzunguko wa kwanza.

Vilevile alieleza kuwa, bei ya umeme vijijini ni shilingi 27,000 tu na kwamba Taasisi za umma kama vile Shule, Zahanati, Misikiti, na Mkanisa zipewe kipaumbele cha kuunganishiwa umeme mara miundombinu ya umeme inapofika katika maeneo husika.

Katika hatua nyingine, Waziri wa Nishati, alisema kuwa mradi wa usambazaji umeme katika vitongoji ambavyo bado havina nishati ya umeme nchini utanza mwezi Julai mwaka huu na utatekelezwa ndani ya miezi 12.

Kwa upande wake, Mbunge wa Mbogwe, Nicodemus Maganga alisisitiza masuala mbalimbali ikiwemo wananchi kuchangamkia fursa za kuunganisha umeme kwa shilingi 27,000 tu na nishati ya umeme kufika kwenye Taasisi za umma kama vile Zahanati na Shule ili kuweza kuleta manufaa.

Akiwa wilayani Mbogwe, mkoani Geita, Waziri wa Nishati pia aliwasha umeme katika Kijiji cha Nyakasaluma ambacho kimesambaziwa umeme kupitia mradi wa usambazaji umeme



Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe, Martha Mkupasi (wa Tatu kutoka kulia), Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Julius Kalolo na Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Amos Maganga na wakiwa katika hafla ya uzinduzi wa Mradi wa Usambazaji umeme vijijini wa Awamu ya Tatu, mzunguko wa Pili uliofanyika katika Kijiji cha Mpakali wilayani Mbogwe, mkoani Geita.

vijijini wa Awamu ya Tatu Mzunguko wa Kwanza.

Kuhusu kazi ya usambazaji umeme vijijini nchini, alisema

kuwa mpaka sasa ni vijiji 1,956 tu ambavyo havijasambaziwa umeme kati ya vijiji 12,268.

Miradi minne kueneza umeme Dodoma



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemuni akizungumza na wananchi katika Kijiji cha Makutupa wilayani Kongwa, Mkoa wa Dodoma kabla ya kuwasha umeme kwenye Kijiji hicho.

Na Teresia Mhagama, Dodoma

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard

Kalemuni amesema kuwa, takriban miradi minne ya umeme inatekelezwa katika Mkoa wa Dodoma kwa lengo la kuhakikisha kuwa maeneo yote ya Mkoa yanapata nishati ya umeme itakayowasaidia wananchi katika shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi.

Waziri wa Nishati

alisema hayo tarehe 2 Mei, 2021 wakati alipofika katika Kijiji cha Makutupa wilayani Kongwa, mkoani Dodoma ili kuwasha umeme kwenye Kijiji hicho ambapo aliambatana na Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Suleiman Serera, Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga na watendaji mbalimbali wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Alitaja miradi hiyo kuwa ni, mradi wa kusambaza umeme vijijini unaoendelea

sasa wa Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Kwanza

ambao unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi mitatu ijayo, mradi wa kupeleka umeme vitongojini, mradi wa kupeleka umeme kwenye maeneo yaliyo karibu na mitaa mijini (Peri-urban) na miradi inayotekelezwa na TANESCO.

“Kwa Mradi wa kusambaza umeme vijijini Dodoma, Serikali imetoa takriban shilingi bilioni 60, mradi wa kupeleka umeme vitongojini Serikali imetoa shilingi bilioni 48.3, kwa mradi wa Peri-Urban Serikali imetoa shilingi bilioni 23 na mradi mwingine unatekelezwa na fedha



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemuni akikata utepe ikiwa ni ishara ya kuwasha umeme katika Kijiji cha Makutupa, wilayani Kongwa, Mkoa wa Dodoma. Kulia kwake ni Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Suleiman Serera.

Miradi minne kueneza umeme Dodoma

kutoka TANESCO kama ilivyo hapa Makutupa.” Alisema Dkt.Kalemani

Kuhusu kazi ya usambazaji umeme vijijini mkoani Dodoma, Dkt.Kalemani alisema kuwa, vijiji 467 vimeshasambaziwa umeme, kati ya vijiji 581 ambayo ni zaidi ya asilimia 81.

Vilevile, kwa Vijiji 114 ambavyo bado havijasambaziwa umeme mkoani Dodoma, alieleza kuwa wakandarasi pamoja na fedha za kusambaza umeme zimepatikana hivyo vijiji husika vitapata umeme ndani ya miezi 18.

Aidha, katika Wilaya Kongwa, alisema kuwa, kuna vijiji 87 na Vijiji ambavyo havina umeme ni vinne tu ambavyo

vitasambaziwa umeme ndani ya miezi mitatu ijayo.

Dkt.Kalemani aliongeza kuwa, kwa vijiji 1974 ambavyo bado havijasambaziwa umeme nchi nzima kati ya vijiji 12,268, wakandarasi wa kusambaza umeme kwenye vijiji hivyo wameshapatikana na wataingia katika maeneo ya kazi wiki ijayo.

Akiwa wilayani Kongwa, Waziri wa Nishati pia alitembelea eneo la Mbande ambalo wananchi wake wamekuwa wakilalamika kuwa kuna nguzo za umeme zilizosimikwa muda mrefu bila wananchi hao kuunganishiwa umeme.

Akiwa katika eneo hilo, Dkt.Kalemani



Kamishna Msaidizi wa Umeme, Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga pamoja na watendaji mbalimbali wa TANESCO wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani (hayupo pichani) wakati akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Makutupa wilayani Kongwa, Mkoa wa Dodoma.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza na wananchi wa eneo la Mbande, wilayani Kongwa, Mkoa wa Dodoma.



Baadhi ya Miundombinu ya umeme katika Kijiji cha Makutupa wilayani Kongwa.

aliahidi kuwa, Mkandarasi, kampuni ya Derm Electric ataanza kuwaunganishia umeme wananchi kuanzia Ijumaa ya tarehe 7 Mei, 2021.

Akizungumza na wananchi wa Makutupa na Mbande, Dkt. Kalemani aliwasisitiza

kutumia umeme kwa matumizi mbalimbali kwani Serikali inatumia fedha nyingi kufikisha umeme katika maeneo mbalimbali nchini pamoja na kupunguza gharama za uunganishaji ili kila mtanzania atumie nishati hiyo muhimu.

WANANCHI WA KISIWA CHA SONGOSONGO WANUFAIKA NA MRADI WA GESI

**Hafsa Omar,
SongoSongo**

Wananchi wa Kisiwa cha

SongoSongo, kilichopo Wilayani Kilwa, mkoani Lindi, wamesema uwepo wa kiwanda cha kuchakata Gesi Asilia cha SongoSongo kimewapa manufaa mengi kijijini humo.

Hayo yalibainishwa na wanakijiji hao kwa nyakati tofauti wakati wa ziara ya watumishi wa Wizara ya Nishati wa Idara ya Petroli na Gesi.

Akizungumza kwa



Afisa Mtendaji wa kata ya Songo Songo, Afkato Masami, Akizungumza wakati wa kikao na Watumishi wa Wizara ya Nishati wa Idara ya Petroli na Gesi (hawapo pichani).

niaba ya wananchi, Afisa Mtendaji wa Kata, Afkato Msami, alisema uwepo wa mradi huo umewawezesha wananchi kunufaika na huduma mbalimbali ambazo zinatolewa

kiwanda hicho.

Alieleza kuwa, manufaa hayo ni pamoja na kupata huduma ya Maji ambayo inatolewa na kiwanda hicho, ambapo alisema hapo awali walikuwa hawapati huduma ya Maji safi na salama.

Pia, amesema kutokana na uwepo wa kiwanda hicho wananchi wamepata fursa ya kupata soko la kuzia bidhaa zao, ambapo kwasasa wamepata wateja wa uhakika wa kuwauzia bidhaa zao zinazotokana na bahari.

Vilevile, alisema kuwa kwasasa wananchi wanajivunia usalama unaopatikana kijijini

humo ambapo uwepo wa askari katika kiwanda hicho umesababisha kutokuwepo kwa matendo ya uhalifu katika maeneo hayo.

Aidha, alisema wananchi pia wanapata huduma ya usafiri ambayo inatolewa na kiwanda hicho.

Naye, Bi. Chiku Ali, alisema wananchi wa kijiji hicho wanaishukuru Serikali kwa kuleta miradi hiyo katika kijiji chao, ambapo kwasasa huduma mbalimbali za kijamii ikiwemo umeme, maji, afya, usafiri zinapatikana ukilinganisha hapo awali.



Mitambo ya kuzalisha Gesi Asilia iliyopo katika kiwanda cha Songo Songo, kilichopo wilayani Kilwa, mkoa wa Lindi.



JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI



Fika Ofisi ya Mawasiliano,
Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au
Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018
Nukushi +255-26-2320148

 www.nishati.go.tz

 [Wizara ya Nishati](https://www.facebook.com/Wizara.ya.Nishati)

 [@Nishati2017](https://twitter.com/Nishati2017)

 [wizara_ya_nishati_tanzania](https://www.instagram.com/wizara_ya_nishati_tanzania)

 [Wizara ya Nishati](https://www.youtube.com/Wizara.ya.Nishati)